**HOTUBA YA IJUMAA**

**الإسراء والمعراج وفرضية الصلاة**

**Israa na Miiraji pamoja na ulazima wa ibada ya swala.**

**Imefasiriwa**

**na**

**profesa Ayman Alasar**

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mola wa ulimwengu Mwenye kusema ndani ya Kitabu chake:

**وَأَقِيمُوا الصَّلاةَ وَآتُوا الزَّكَاةَ وَارْكَعُوا مَعَ الرَّاكِعِين.**

´ {**Na shikeni Sala, na toeni Zaka, na inameni pamoja na wanao inama**}. Ninashuhudia kuwa hakuna mola wa haki isipokuwa ni Mwenyezi Mungu peke yake hana mshirika, na ninashuhudia kuwa Mtume wetu Muhammad ni mja wake na Mtume wake, ewe Mwenyezi Mungu peleka rehma amani na baraka kwake na kwa watu wa nyumbani kwa na Maswahaba zake na wale wote wenye kuwafuata kwa wema mpaka siku ya malipo.

Baada ya Utangulizi….

Safari ya Israa na Miiraji ilikuwa imejaa karama za Mwenyezi Mungu na utoaji wa Kimungu ambao Mwenyezi Mungu Mtukufu alihusisha kwa umma huu, kubwa katika utoaji huo ni umma kupewa ibada ya swala, kwani ni zawadi ya kimungu ambayo inamuunganisha mja na Mola wake Mtukufu, ambapo Mtume wetu anasema S.A.W: “*Nikafaradhishiwa swala hamsini usiku na mchana, hivyo nikateremka kwa Nabii Musa A.S akaniuliza: Mola wako amekupa nini kwa ajili ya Umma wako? Nikamjibu: Nimepewa swala hamsini. Nabii Musa akaniambia rudi tena kwa Mola wako na muombe akupunguzie kwani watu wako hawataweza kuzitekeleza…Nikasema: Ewe Mola wangu naomba uwapunguzie watu wangu, hivyo Mtume wetu hakuacha kumrudia Mola wake mpaka mwisho Mwenyezi*

*Mungu Akasema kumwambia Mtume: Basi ni swala tano kwa kila siku na kila swala moja ina malipo ya swala kumi na kufanya swala zile zile hamsini*".

Na Mtume kupewa ibada ya swala ndani ya usiku wa Miiraji akiwa uwingu wa saba ni dalili ya nafasi yake ya juu, kwani ibada ya swala ni kitulizo cha macho na uhai wa moyo pamoja na ladha ya roho, nayo ni ngazi ya kiimani wanayopandia watu katika kutafuti viwang ovya ukaribu kwa Mola wa viumbe, ambapo Mola Mtukufu Anasema:

**وَاسْجُدْ وَاقْتَرِبْ**

{**Sujudu na jiweka karibu**},

na Mtume wetu anasema:

**أَقْرَبُ ما يَكونُ العَبْدُ مِن رَبِّهِ، وهو ساجِدٌ**

"*Kipindi cha mja kuwa karibu zaidi na Mola wake ni pale anapokuwa amesujudu*".

Na Mtume S.A.W anasema:

**عَلَيْكَ بِكَثْرَةِ السُّجُودِ، فَإِنَّكَ لا تَسْجُدُ للهِ سَجْدَةً إلا رَفَعَك اللهُ بِهَا دَرَجةً، وَحطَّ بِهَا عَنْكَ خَطِيئَةً.**

"*Ni juu yako kusujudu kwa wingi, kwani haumsujudii Mwenyezi Mungu sijida ispokuwa Mwenyezi Mungu hukuinua daraja na kufutiwa madhambi*".

Kama vile kuletwa ibada ya swala ndani ya safari ya Miiraji ni liwazo kwa Mtume wetu Muhammad S.A.W baada ya kufikiwa na mitihani migumu ndani ya mwaka huo ambao uliitwa mwaka wa huzuni, katika hili kuna ishara kuwa ibada ya swala ni sababu ya utulivu wa moyo na kufunguka kifua pamoja utulivu wa macho, yenyewe ni msaada wa Mwenyezi Mungu Mtukufu katika shida mbalimbali, ambapo Mwenyezi Mungu Anasema:

**وَلَقْد نَعْلَمُ أَنَّكَ يَضِيقُ صَدْرُكَ بِمَا يَقُولُونَ* فَسَبِّحْ بِحَمْدِ رَبِّكَ وَكُنْ مِنَ السَّاجِدِينَ * وَاعْبُدْ رَبَّكَ حَتَّى يَأْتِيَكَ اليَقِينُ.**

{**Na Sisi tunajua kwa hakika kuwa wewe kifua chako kinaona dhiki kwa hayo wayasemayo * Basi mtakase Mola wako Mlezi kwa kumhimidi, na uwe miongoni wanao msujudia * Na muabudu Mola wako Mlezi mpaka ukufikie uyakinifu**}.

Na Mwenyezi Mungu Anasema tena:

**وَاسْتَعِينُوا بِالصَّبْرِ وَالصَّلَاة**

{**Na tafuteni msaada kwa kusubiri na kwa kuswali**}.

Na Mtume S.A.W anasema:

**وجُعِلَت قُرَّةُ عَيني في الصَّلاةِ.**

"*Na nimefanyiwa kitulizo cha macho yangu ni ndani ya swala*".

Na Mtume alikuwa anamwambia Swahaba Bilali R.A:

**يَا بِلالُ، أَقِمِ الصَّلاةَ، أَرِحْنا بها**

"*Ewe Bilal, kimu swala, tustereheshe kwayo*".

Na Mwenyezi Mungu kupunguza ibada ya swala kwa watu wa Muhammad ni ubainifu wa ukamilifu wa huruma yake Mola Mtukufu kwa waja wake, na ni dalili inayosifika nayo kwa upekee Sharia ya Kiislamu ya wepesi na kuondoa uzito, ambapo Mwenyezi Mungu Anasema: **لاَ يُكَلِّفُ اللهُ نَفْسًا إِلاَّ وُسْعَهَا** {**Mwenyezi Mungu haikalifishi nafsi yeyote ila kwa kadiri ya iwezavyo**}. Na Mola Anasema tena:

**يُرِيدُ اللَّهُ بِكُمُ الْيُسْرَ وَلاَ يُرِيدُ بِكُمُ الْعُسْرَ.**

{**Mwenyezi Mungu anakutakieni yaliyo mepesi wala hakutakieni yaliyo mazito**}.

Na Mtume S.A.W anasema:

**إِنَّ الدِّينَ يُسْرٌ**

“*Hakika dini ni nyepesi*”.

Na Mtume S.A.W anasema tena:

**إِنَّ اللهَ لَمْ يَبْعَثْنِي مُعَنِّتًا ولا مُتَعَنِّتًا، وَلَكِنْ بَعَثَنِي مُعَلِّمًا مُيَسِّرًا**

“*Hakika Mwenyezi Mungu hakunituma kuleta amri kali wala kuleta uzito, bali amenileta kuwa mwalimu na mrahisishaji*”.

****

**HOTUBA YA PILI**:

Shukrani zote anastahiki Mwenyezi Mungu Mlezi wa viumbe, rehma na amani zimwendee Nabii wa mwisho naye ni Mtume Muhammad S.A.W pamoja na watu wa nyumbani kwake na Maswahaba zake wote.

Hakuna shaka kuwa ibada ya swala na mazungumzo kati ya watu na Muumba wao Mtukufu, ambapo Mtume S.A.W anasema:

**قَالَ اللهُ تَعَالَى: قَسَمْتُ الصَّلَاةَ بَيْنِي وَبَيْنَ عَبْدِي نِصْفَيْنِ، وَلِعَبْدِي مَا سَأَلَ، فَإِذَا قَالَ الْعَبْدُ: {الْحَمْدُ للهِ رَبِّ الْعَالَمِينَ}، قَالَ اللهُ تَعَالَى: حَمِدَنِي عَبْدِي، وَإِذَا قَالَ: {الرَّحْمَنِ الرَّحِيمِ}، قَالَ اللهُ تَعَالَى: أَثْنَى عَلَيَّ عَبْدِي، وَإِذَا قَالَ: {مَالِكِ يَوْمِ الدِّينِ}، قَالَ: مَجَّدَنِي عَبْدِي، فَإِذَا قَالَ: {إِيَّاكَ نَعْبُدُ وَإِيَّاكَ نَسْتَعِينُ}، قَالَ: هَذَا بَيْنِي وَبَيْنَ عَبْدِي، وَلِعَبْدِي مَا سَأَلَ، فَإِذَا قَالَ: {اهْدِنَا الصِّرَاطَ الْمُسْتَقِيمَ صِرَاطَ الَّذِينَ أَنْعَمْتَ عَلَيْهِمْ غَيْرِ الْمَغْضُوبِ عَلَيْهِمْ وَلاَ الضَّالِّينَ}، قَالَ: هَذَا لِعَبْدِي وَلِعَبْدِي مَا سَأَلَ.**

“Mwenyezi Mungu amesema: Nimeigawa swala kati yangu na mja wangu nusu mbili, na mja ni kutokana na anachoomba, pindi mja anaposema: {**Sifa njema zote ni za Mwenyezi Mungu, Mola Mlezi wa viumbe vyote**} Mwenyezi Mungu anasema: Mja wangu amenishukuru, pindi mja anaposema: {**Mwingi wa Rehema Mwenye Kurehemu**} Mwenyezi Mungu husema mja wangu amenisifu, na pindi mja anaposema: {**Mwenye Kumiliki Siku ya Malipo**}. Mwenyezi Mungu husema

mja wangu amenitukuza, na pindi mja anaposema: {**Wewe tu tunakuabudu, na Wewe tu tunakuomba msaada**}. Mwenyezi Mungu husema, hili ni kati yangu na mja wangu, na mja wangu alichoomba, pindi mja akisema: {**Tuongoe njia iliyo nyooka Njia ya ulio waneemesha, siyo ya walio kasirikiwa, wala walio potea**}. Mwenyezi Mungu husema, hili ni kwa ajili ya mja wangu na mja wangu alichoomba.

Kama vile ibada ya swala ina athari ya ajabu katika kuijenga nafsi kwenye maadili mema na tabia nzuri pamoja na kuipamba na maadili mazuri, ambapo Mwenyezi Mungu Anasema:

**وأقم الصلاة إِنَّ الصَّلَاةَ تَنْهَى عَنِ الْفَحْشَاءِ وَالْمُنْكَرِ**

{**Na ushike Sala. Hakika Sala inazuilia mambo machafu na maovu**}

mtu mwenye kuswali kweli haiwezekani kwake kuwa mtu muwongo, wala mwenye kughushi mambo, wala kuwa mdanganyifu, wala msaliti, wala mwenye hila mbaya, wala mwenye kukiuka makubaliano, bali anakuwa ni maadili mema yanayotembea ardhini kwa mujibu wa mfumo wa Mwenyezi Mungu na Sharia zake.

**Ewe Mwenyezi Mungu tunakuomba utujaalie wenye kudumisha ibada ya swala sisi na kwa vizazi vyetu, ewe Mola wetu tukubalie maombi.**

**Aamin**